

# BODI YA USAJILI WA MAKANDARASI (CRB)



## MKUTANO WA MASHAURIANO NA WADAU WA SEKTA YA UJENZI KWA MWAKA 2025

*“Ukuaji wa Makandarasi wa ndani; Fursa na Changamoto”*

Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) inapenda kuwataarifu **Makandarasi** na wadau wote wa Sekta ya Ujenzi wakiwemo **Waajiri, Wataalam Washauri** (Wahandisi, Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi), wataalam mbalimbali katika sekta ya ujenzi na watunga sera kuwa imeandaa mkutano wa mashauriano na wadau wa sekta ya ujenzi utakaofanyika Jijini **Dar es Salaam** kuanzia **Tarehe 15 – 16 Mei 2025, Ukumbi wa Diamond Jubilee**. Mkutano utaanza saa **2.00 asubuhi**. Kaulimbiu ya mkutano ni: *“Ukuaji wa Makandarasi wa ndani; Fursa na Changamoto”*. *Mada zifuatazo zitajadilwa:-*

- Jitihada za serikali katika kukuza Makandarasi wa ndani.
- Mazingira ya ukuaji wa Makandarasi wa ndani kupitia sheria ya ununuzi wa umma ya mwaka 2023 na kanuni zake za mwaka 2024.
- Mtazamo wa Makandarasi kuhusu mazingira ya ukuaji wa Makandarasi wa ndani.
- Mazingira na fursa za kifedha kwa Makandarasi wa ndani
- Mambo ya kuzingatia kuepuka changamoto za kikodi katika biashara
- Elimu ya Afya, Fedha na Uwekezaji
- Matumizi ya TEHAMA katika ukandarasi
- Uzoefu wa wataalam wa ndani kuhusu utekelezaji wa miradi kwa ufanisi

<b>Walengwa</b>	Makandarasi, Wataalam washauri; Wabunifu Majengo, Wakadiriaji Majenzi, Watunga Sera, Wasimamizi wa sheria mbalimbali zinazoathiri sekta ya ujenzi, Wahandisi, Wataalam wanaoshabihiana nao, Waajiri, Watunga sera za uwezesaji wananchi kiuchumi na wadau wote wa Sekta ya Ujenzi wanaalikwa kushiriki.
<b>Ada ya Ushiriki</b>	Ada ya ushiriki ni <b>TZS 75,000/=</b> kwa Makandarasi na Wadau wengine. Ada itagharomia mahitaji ya mkutano kama ukumbi, chakula na vinywaji kwa siku mbili (2) za mkutano.  <b>Ada ya ushiriki italipwa kwa utaratibu ufuatao:-</b> Malipo ya ada ya ushiriki yafanywe kupitia benki ya <b>CRDB Plc, NBC Ltd.</b> au <b>NMB Plc</b> kwa jina la <b>CONTRACTORS REGISTRATION BOARD</b> . Pia kwa kupitia mitandao ya simu kwa kutumia <b>“Control Number” 995740124352</b>  Hakikisha <b>namba ya simu ya mshiriki</b> imeoneshwa katika karatasi ya malipo ya benki.
<b>Jinsi ya Kujisajili</b>	Washiriki wathibitishe kuhudhuria mkutano kwa kulipa ada ya ushiriki mapema kabla ya tarehe ya mkutano na kutuma majina na mawasiliano yao katika ofisi yoyote ya <b>CRB</b> nchini. <b>Washiriki wanahimizwa kujisajili mapema ili kuepuka usumbufu unaoweza kujitokeza.</b>
<b>Mafunzo endelevu (PDU)</b>	Washiriki ambao ni wataalam wa fani za ujenzi watatuzwa alama za mafunzo endelevu zitakazotolewa na Bodi zao za usajili.

**Kwa taarifa zaidi fanya mawasiliano kama ifuatavyo:-**

**CRB Makao makuu**, S.L.P 96 Dodoma Simu 026 2962403/4, Tovuti: [www.crb.go.tz](http://www.crb.go.tz),

Barua pepe: [crbhq@crb.go.tz](mailto:crbhq@crb.go.tz)

**CRB Kanda ya Mashariki**, S.L.P 33621 Dar es Salaam Simu 022 2137962-3, Barua pepe: [crbez@crb.go.tz](mailto:crbez@crb.go.tz)

**CRB Kanda ya Ziwa**, S.L.P 2815 Mwanza Simu 028 2500218, Barua pepe: [crblz@crb.go.tz](mailto:crblz@crb.go.tz)

**CRB Kanda ya Kusini**, S.L.P 1690 Mbeya Simu 025 2502480, Barua pepe: [crbsz@crb.go.tz](mailto:crbsz@crb.go.tz)

**CRB Kanda ya Kaskazini**, S.L.P 16795 Arusha Simu 027 2520167, Barua pepe: [crbnz@crb.go.tz](mailto:crbnz@crb.go.tz)

**CRB Kanda ya Kati**, S.L.P 2618 Dodoma Simu 026 2962405, Barua pepe: [crbcz@crb.go.tz](mailto:crbcz@crb.go.tz)